THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

021 **KISWAHILI**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

MUDA: Saa 3 ***Alhamisi 9 Oktoba 2008 mchana***

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B, D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni la lazima.

3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org

Mtihani huu na mitihani mingine yanapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

SEHEMU A (alama 10)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

UFAHAMU

1. Soma habari ifuatayo kwa makini na kisha jibu maswali yanayofuata:

Wimbi la kusakama wahamiaji kutoka nchi jirani, hasa vijana wenye kazi, limeshika kasi katika miji mbalimbali nchini Afrika Kusini. Watu arobaini wameripotiwa kuuawa hadi sasa, mamia wamejeruhiwa, baadhi wakiwa wamechomwa moto. Vijana wenye mapanga, visu, nondo, nyundo na mishale wanawasaka mahamiaji majumbani, ofisini na mitaani.

Ghasia hizo zinatokana na vijana wa Afrika kusini kudai kwamba wanakosa ajira kwa sababu nafasi zao zinachukuliwa na wageni na wao kubaki wanazurura mitaani bila ya kazi. Wimbi hilo la vurugu na mauaji limeiharibia sifa Afrika Kusini nchi ambayo ilifikia hapo ilipo kwa msaada mkubwa wa hali na mali wa nchi za kusini mwa Afrika. Watu wa Afrika Kusini wamesahau kwamba wakati wa utawala wa makaburu, nchi jirani ziliwapokea maelfu kwa maelfu ya vijana na wazee wa Afrika Kusini kuwapa hifadhi pamoja na kusaidia mikakati ya mapambano dhidi ya makaburu. Pia vijana wa nchi hizo walikosa nafasi za masomo ya juu kutokana na wakimbizi wa Afrika Kusini kupewa upendeleo katika shule za sekondari na vyuo vikuu vya nchi hizo. Lakini leo hii watu wa nchi hizi wanaonekana si lolote si chochote nchini Afrika ya Kusini.

Hivi sasa vijana wengi wamekosa ajira katika nchi za Zimbabwe, Msumbiji, Malawi na hata Tanzania kwa vile makampuni ya Afrika ya Kusini yamechukua makampuni makubwa ya nchi hizo kama vile viwanda vya bia, mabenki na huajiri watu kutoka Afrika Kusini kufanya kazi huko. Suala hilo limehamasisha kukimbilia Afrika Kusini kwa vijana wengi ili kupata ajira.

Sasa njia pekee iliyobaki kwa vijana wa nchi jirani wasiokuwa na kazi ni kuzifuata ajira hizo Afrika Kusini. Wageni, hasa kutoka nchi za Afrika, wamekuwa wakikutana na vikwazo vya kupata vibali vya kufanya kazi, lakini wamekuwa wakitumia njia za panya kupata ajira. Vijana wengi wa Afrika Kusini wamekuwa wakikosa ajira kutokana na elimu ndogo au maambukizi ya virusi vya UKIMWI yaliyozagaa nchini humu ukilinganisha na nchi jirani.

Takwimu za serikali, kwa mfano, zinaonesha zaidi ya asilimia thelathini (30%) ya wafanyakazi wa kwenye bandari ya mji wa Durban na maeneo ya ukanda wa Pwani, wanaishi na virusi vya UKIMWI na makampuni ya maeneo hayo yamekuwa yakibagua katika ajira maana uwezo wa watu hao kufanya kazi za sulubu ni mdogo kwa sababu ya UKIMWI.

Kwa ujumla ghasia zimezusha wasiwasi mkubwa kwa Afrika Kusini, nchi ambayo inakabiliwa na maandalizi ya kuwa mwenyeji wa michuano ya fainali za Kombe la Dunia kwa mchezo wa soka mwaka 2010. Inatarajiwa kuvutia wageni wapatao nusu milioni. Wasiwasi unakuja kwa vile kiasi kikubwa cha fedha kimetumika katika maandalizi na faida yake inatarajiwa kupatikana wakati wa mashindano hayo. Hivyo vitendo vya mauaji vinatia doa. Upo uwezekano wa kukosa nafasi hiyo kutokana na kuhofia usalama na amani kwa wanamichezo.

Mtihani huu na mitihani mingine yanapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

Maswali

(a) Kichwa cha habari hii kinachofaa ni kipi?
(b) Vijana wengi kusini mwa Afrika wamemiminika Afrika Kusini ili wapate ajira. Eleza mambo **mawili (2)** yaliyosababisha vijana hao wapate ajira Afrika ya Kusini.
(c) Ungeishauri nini serikali ya Afrika ya Kusini?
(d) Makampuni yanahofia kuwaajiri vijana wa Afrika Kusini. Ipi sababu kubwa ya hofu hiyo?

2. Andika ufupisho wa aya mbili za mwisho za habari uliyoisoma kwa maneno **hamsini (50)**.

SEHEMU B (alama 25)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

3. Viambishi awali na viambishi tamati vina uwezo wa kubadili umbo na maana ya neno. Katika maneno yafuatayo eleza dhima ya kila kiambishi.
   (a) Watakapotupambanisha.
   (b) Sielekezi.

4. Upatanisho wa kisarufi hufanya nomino mbalimbali kuwa katika kundi moja. Fikiria nomino tano na kwa kutumia sentensi moja kwa kila nomino zipange katika makundi yake.

5. Uchanganuzi wa sentensi hufanyika hatua kwa hatua. Ukitumia hatua hizo changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali.

   Wale wawili watakuwa wamepimwa virusi vya UKIMWI hivyo afya zao zitakuwa nzuri.

6. Eleza njia zilizotumika kuunda misamiati ifuatayo katika lugha ya Kiswahili.
   (a) Sigara.
   (b) Mwanajeshi.
   (c) Kipima pembe.
   (d) Pembe tatu.
   (e) Mtutu.

7. “Vitenzi vifuatavyo vinatofautiana kiasili”. Toa sababu za kuthibitisha jibu lako, kisha vipange vitenzi hivyo kutegemeana na uasili wake.

(a)	Lima	(b)	Arifu	(c)	Ruka	(d)	Sali	(e)	Pamoja
(f)	Adhibu	(g)	Weka	(h)	Buni	(i)	Stahimili	(j)	Chambua.

Mtihani huu na mitihani mingine yanapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

SEHEMU C (alama 10)

Jibu swali **moja** kutoka sehemu hii.

UANDISHI

8. Muundo wa uandishi wa barua za kirafiki na barua za kikazi ni tofauti. Thibitisha kauli hiyo.
9. Manyanda akiwa mfanyakazi wa kiwanda cha korosho Tanita alipewa taarifa kuhusu ugonjwa wa baba yake. Wewe kama Manyanda andika barua ya kuomba ruhusa. Anuani ya kiwanda ni S.L.P. 1030, Kibaha.

SEHEMU D (alama 10)

Jibu swali la **10.**

MAENDELEO YA KISWAHILI

10. Eleza jinsi shughuli za Waarabu zilivyosaidia kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kabla ya uhuru.

SEHEMU E (alama 45)

Jibu maswali **matatu** katika sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

FASIHI KWA UJUMLA

11. “Ngonjera na majigambo ni vipera vya fasihi simulizi vinavyofanana kimuundo na kiuwasilishaji”. Kubali au kataa kauli hii.

12. “Mshairi ni mhakiki wa jamii”. Kwa kutumia vitabu teule **viwili (2)** vya ushairi ulivyosoma, jadili kauli hii.

13. “Jina la kitabu ni kivutio cha wasomaji wa riwaya”. Kwa kutumia riwaya teule **mbili (2)** ulizosoma linganisha majina ya vitabu jinsi yanavyosadifu yaliyomo.

14. “Waandishi wengi huandika kazi zao kwa lengo la kutoa ujumbe katika jamii”. Kwa kutumia tamthiliya **mbili (2)** zilizoorodheshwa, thibitisha ukweli wa kauli hii.

15. “Tenzi zina kanuni maalumu”. Tunga utenzi wenye beti **tatu (3)** unaohusu ugonjwa wa UKIMWI.

Mtihani huu na mitihani mingine yanapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org

ORODHA YA VITABU

Ushairi

Diwani ya Mloka	- C. Mloka (B.P)
Malenga Wapya	- TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka	- T.A. Mvungi (EP & DLTD)

Riwaya

Kusadikika	- S. Robert (E.P)
Watoto wa Mama N'tilie	- E. Mbogo (H.P)
Kiu ya Haki	- Z. Mwanga (R.P.)

Tamthiliya

Mfalme Juha	- F. Topan (DUP)
Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe	- E. Semzaba (ESC)
Kilio Chetu	- Medical Aid Foundation (TPH)

Mtihani huu na mitihani mingine yanapatikana kwenye tovuti yetu: http://maktaba.tetea.org